## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

## WAKALA WA HUDUMA YA UNUNUZI SERIKALINI (GPSA)

# TANGAZO LA AJIRA YA MUDA (*MARUDIO*)

Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 na kuzinduliwa rasmi tarehe 16 Juni, 2008.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini anayofuraha kuwatangazia wananchi wote wa Tanzania nafasi za Ajira ya Mkataba kwa nafasi ya Dereva na Msaidizi wa Ofisi kama ifuatavyo;

**A.** **Dereva**: Lori tani 50 (Tanker) nafasi 3, Gari ya abiria 28-32 (COASTER) nafasi 4.

Kituo cha Kazi: Ofisi ya Makao Makuu.

**Majukumu ya Kazi:**

1. Kuendesha gari la Wakala kwenda mahala palipoidhinishwa.
2. Kukagua gari kabla ya kuondoka na baada ya kufika safari.
3. Kutoa taarifa pale gari linapokuwa na hitilafu.
4. Kuliweka gari katika hali ya usafi.
5. Kulifanyia gari matengenezo madogo madogo yatakapohitajika.
6. Kutunza taarifa zote za safari katika ***logbook.***
7. Kutekeleza majukumu mengine atakayopangiwa.

**Sifa na Masharti ya Mwombaji:**

1. Awe amehitimu Elimu ya Sekondari ya kidato cha nne.
2. Awe amefaulu mafunzo ya Udereva katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)
3. Awe na Leseni ya udereva daraja E au C kwa dereva wa lori.
4. Awe na Leseni ya udereva daraja C1 au C kwa dereva wa gari ya abiria (COASTER).
5. Awe na umri kati ya miaka 18 hadi 45.
6. Mwombaji asiwe mwenye kesi au tuhuma za uhalifu.
7. Mwombaji awe amesajiliwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
8. Awe tayari kufanya kazi muda wote ikiwemo siku za sikukuu na mapumziko.

9. Mwombaji wa nafasi ya udereva aainishe katika barua aina ya gari anayoomba kuendesha.

**B.** **Msaidizi wa Ofisi:** nafasi 1.

Kituo cha Kazi: Ofisi ya Makao Makuu.

**Majukumu ya Kazi:**

1. Kufanya Usafi wa Ndani ya Maghala.
2. Kufanya Usafi wa Nje ya Maghala.
3. Kutengeneza Bustani nje ya Maghala na kuzitunza.
4. Kufanya Usafi wa Ofisi za Makao Makuu kila Ijumaa ya mwisho ya kila mwezi.

**Sifa na Masharti ya Mwombaji;**

1. Awe amehitimu Elimu ya Sekondari ya kidato cha nne.
2. Awe na umri kati ya miaka 18 hadi 45.
3. Mwombaji asiwe mwenye kesi au tuhuma za uhalifu.
4. Mwombaji awe amesajiliwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
5. Awe tayari kufanya kazi muda wowote ikiwemo siku za sikukuu na mapumziko.

**Nyaraka muhimu za kuwasilisha wakati wa kutuma maombi:**

1. Nakala ya Cheti cha kuzaliwa;
2. Nakala za vyeti vya shule na Taaluma;
3. Nakala ya kadi/namba ya kitambulisho cha Taifa;
4. Leseni ya Udereva kwa mwombaji wa nafasi ya dereva;
5. Barua ya utambulisho kutoka Serikali ya mtaa anakoishi;
6. Uthibitisho wa Polisi ya kuwa ni raia mwema na hajawahi kuwa na makossa yoyote ya jinai kwa mwombaji wa nafasi ya dereva;
7. Taarifa ya Daktari (kutoka Hospitali inayotambuliwa na Serikali) kuonesha kuwa hana matatizo ya macho kwa mwombaji wa nafasi ya dereva;
8. Picha mbili za rangi (passport size);
9. Taarifa binafsi za mwombaji (CV) na majina mawili ya wadhamini.
10. Nyaraka zote zishuhudiwe na Wakili/Hakimu.

**Namna ya kuwasilisha maombi:**

Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya mkono katika Ofisi ya Wakala Makao Makuu kuanzia tarehe **29/12/2021** hadi tarehe **11/01/2022** kupitia anuani ifuatayo;

Afisa Mtendaji Mkuu,

Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini,

S.L.P. 9150,

DAR ES SALAAM.

Imetolewa na

**Afisa Mtendaji Mkuu**

**WAKALA WA HUDUMA YA UNUNUZI SERIKALINI**

29/12/2021